

# Mwelekeo

## Usimamizi wa Biashara na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika wa Kidijitali kwa Wanawake Wajasiriamali Wadogo

*Ripoti hii imeweza kufanikishwa kwa ushirikiano wa ukarimu na watu wa Marekani kupitia Uwakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID). Muongozo huu ulitolewa chini ya Mradi wa Frontia za Kidijitali za DAI (Cooperative Agreement AID-OAA-A-17-00033) kutokana na ombi la USAID wakishirikiana na Mastercard.*

# Taaswira ya Moduli

## Jedwali la yaliyomo


**Sehemu ya 1:** Utangulizi wa mafunzo na wahusika — 4

**Sehemu ya 2:** Kuwa na Maono — 22

**Sehemu ya 3:** Kuelewa biashara rasmi na zisizo rasmi — 29

**Sehemu ya 4:** Kuendesha tathmini ya mapungufu kwenye duka lako — 34


## Malengo

1. Kujifunza kuhusu masomo yanayopatikana kwenye mafunzo haya.
2. Kuelewa hali halisi iliyopo ya biashara yako.
3. Kuwa na maono ya biashara yako
4. Tambua elimu na ujuzi unaohitaji kukuza biashara yako.

## Kwenye Moduli hii, unaweza…

- ✓ kutaka kujua wahusika wa mafunzo na kikundi chako cha mafunzo
- ✓ kutathmini hali halisi ya biashara yako
- ✓ kuchanganua maeneo yanayohitaji kuboreshwa

# SEHEMU YA 1: UTANGULIZI WA MAFUNZO NA WAHUSIKA

**Malengo:**

1. Kujifunza kuhusu malengo ya haya mafunzo.
2. Kuelewa ujuzi unaoweza kupata kutoka kwa haya mafunzo.
3. Ili kutaka kujua wahusika wa mafunzo na kikundi chako cha mafunzo.



# Malengo ya Haya Mafunzo

Kuwa na wateja wako wa kutosha na mapato kwa kuboresha ujuzi wa kusimamia biashara yako.

Kuwa na motisha ya ujasiriamali wako, uwezo, na ujuzi kupitia mafunzo ya biashara na ujuzi wa kuzoma na kuandika kidijitali.

Kujifunza jinsi ya kutumia huduma za kifedha na simu yako kwenye uendeshaji wa biashara yako na shughuli za kifedha.


# Moduli za Mafunzo



# Baada ya Haya Mafunzo, Utajua…



Kutumia kitabu kuweka hesabu na usimamizi wa kifedha ili kufuatilia na kuweka rekodi za utendaji wa biashara yako.



Kuimarisha jukumu lako katika usimamizi wa biashara yako.



Kuongeza ufahamu wako na kukubali kutumia vifaa vya kidijitali na malipo.



Kuongeza uwezo wako wa kufikia huduma za kifedha, kama vile mkopo na bima.

# Sasa Tufahamiane!



Ni watu wangapi wanaishi nyumbani kwako?

Umeolewa? Una mtoto yeyote?

Unaendesha duka la aina gani?

Ni bidhaa ngapi unauza kwa siku?


Ni bidhaa zako zipi zinazopendwa sana?

Biashara yako imesajiliwa na serikali?
Una leseni ya biashara? (hiari)



## ONYESHO LA 1

Sasa tukutane na Imani na tufuatilie safari yake wakati anapotumia ujuzi aliojifunza kwa haya mafunzo ili kuboresha na kukuza biashara yake.



## ONYESHO LA 2



Hujambo! Jina langu ni Imani. Namiliki na naendasha hili duka.

## ONYESHO LA 3



Miaka mitano iliyopita, mume wangu aliugua. Hapo nikawa na jukumu la kuwatunza wanangu watatu na wakwe wangu ambao wamezeeka. Ilinibidi kung’ang’ana na majukumu yangu ya nyumbani pamoja na kuendesha duka langu. Kila siku ilikuwa ni kupambana.

## ONYESHO LA 4



Nilipochukua hatamu ya kuendesha duka, duka lilikuwa linapoteza pesa. Mauzo yalikuwa kidogo, na kila siku, wateja wachache walikuwa wanakuja dukani kwangu. Sikujua jinsi ya kufuatilia bidhaa zangu au kusimamia bili zangu. Sikujua nifanye nini kukuza biashara yangu.

## ONYESHO LA 5

Basi nikaamua kufanya haya mafunzo.Yalinipatia ufahamu wa jinsi ya kusimamia fedha na uendeshaji wa biashara yangu, na yakanisaidia kuwa na ujuzi mpya ambao sasa nautumia kuendesha na kukuza biashara yangu.



# ONYESHO LA 6



Nilihudhuria mafunzo ya biashara pamoja na wanabiashara wenzangu wa kike wa jamii yangu. Hata baada ya mafunzo, tunaendelea kusaidiana.

## ONYESHO LA 7



## ONYESHO LA 8


Niliboresha duka langu, Nikaongeza bidhaa dukani kulingana na mahitaji ya wateja, nikaanza kukubali malipo ya kidijitali, na kuboresha uhusiano mwema kwa wateja wangu na usimamizi wa kifedha.

# ONYESHO LA 9



Pole pole, wateja zaidi wakaanza kuja dukani kwangu kununua bidhaa, na duka langu likaanza kupata faida.

## ONYESHO LA 10



## ONYESHO LA 11

Hiyo ndiyo ilikuwa safari yangu. Haya mafunzo yamenisaidia kuendesha na kukuza duka langu. Ikiwa mimi naweza kufanya, hata wewe unaweza!




Sasa tujadiliane!
Ni kipi kilikuvutia sana?
Ni vipengele gani kwenye hadithi unaweza kuelezea, na kwanini?
Ni sehemu gani ya hadithi ilikuwa tofauti na maisha yako binafsi?

# SEHEMU YA 2:
# KUWA NA MAONO

**Malengo:**

1. Kujifunza jinsi ya kuwa na maono ya biashara yako.
2. Kuelewa jinsi ya kutambua wajibu wako kwenye biashara yako.




# Duka lako linaonekana vipi sasa?

- Wateja wangapi wanakuja dukani kwako kila siku?
- Unauza bidhaa mbalimbali?
- Unatumia mfumo gani wa malipo?
- Ushawahi kutumia mkopo? Unawaruhusu wateja kulipa kwa mkopo?
- Unatumia mbinu gani za kuweka hesabu?
- Duka lako limesajiliwa na serikali?



## Unatarajia duka lako kufikia kiwango gani miaka mitano ijayo?

## Utaendesha vipi biashara?



## Maono yako ya biashara ni yapi?

## Maono yako ni yapi ya wajibu kwenye kuendesha duka?



# Wajibu wako una ushawishi gani kwenye Biashara?

- Unajihusisha kufanya maamuzi kwenye biashara yako? Ungependa kujihusisha zaidi?
- Kama mwanamke unajihisi kuna mipaka umewekewa kufanya kile ambacho ungefanyia biashara? Nini kinahitajika kufanyika ili kubadilisha mipaka hiyo?
- Jinsia yako ina athiri jinsi ambavyo wateja wanatambua duka lako? Kivipi?



## Unaona kuna mgawanyiko wa kijinsia kwenye kufanya maamuzi ya biashara yako na maisha ya nyumbani?




**Haya ni baadhi ya maamuzi yaliyofanywa na wanawake na wanaume katika kiwango cha nyumbani na kwenye biashara:**

- Chakula gani kinapikwa nyumbani
- Vipi au ikiwa watoto wanahitaji kwenda shule
- Kuamua kuuza au kununua ardhi, nyumba na mali.
- Ni bidhaa gani unazouza dukani
- Jinsi ya kupamba au kupanga dukani
- Nani anasimamia hesabu dukani
- Wakati na jinsi ya kutumia simu
- Nani anasimamia fedha za nyumbani na shughuli za biashara za kifedha
- Kuamua kuwekeza na kuweka akiba

- Je, orodha hii inaakisi tabia zako mwenyewe kwenye familia yako na kuendesha duka?
- Unajisikiaje ukiangalia hii orodha ya maamuzi kama mwanamume au mwanamke? Ni haki? Kwanini? Kwanini sio haki?
- Unatamani wajibu wako katika familia yako na biashara ungekuwa tofauti? Kwanini?
- Tunaweza kufanya kazi vipi ili kuleta mabadiliko?



# SEHEMU YA 3
# KUELEWA BIASHARA RASMI NA ISIYO RASMI




**Malengo:**

1. Kutambua hatua zinazohitajika ili kuwa na biashara rasmi.
2. Kuelewa kodi zinazotumika kwenye biashara yako.
3. Kujifunza kuhusu usaidizi unaotolewa na serikali kwa biashara ndogo ndogo.

# Je, Unahitaji Kusajili au Kupata Leseni ya Biashara Yako?

Biashara inaweza kuwekwa  kama rasmi au isiyo rasmi. Sasa tufafanue hiyo inamaana gani, na ni aina gani ya biashara ni bora kwako wewe.

| BIASHARA RASMI | BIASHARA ISIYO RASMI |
|---|---|
| • Huanzishwa kama kitu cha kisheria tofauti na nyumbani kwako | • Inaendeshwa na wewe au familia bila kuwa na sheria tofauti za shirika |
| • Husajiliwa na kupewa leseni na serikali | • Haijasajiliwa au kupewa leseni na serikali |
| • Inastahili kupata mkopo wa biashara ya duka | • Mkopo wa biashara unahitajika kuchukuliwa na wewe mwenyewe |
| • Hubainika wazi tofauti kati yako na biashara | • Haina tofauti kati yako na biashara |
| • Inastahili kupata program za serikali na usaidizi wa biashara ndogo ndogo, kama vile msaada wa fedha | • Haiwezi kupata program za serikali zinazotoa faida kwa walipa kodi |
| • Iwe na Uwezo wa kukata bima | |
| • Lazima ilipe kodi na ada | |

# Unahitajika kufanya nini ili Kusajili au Kupata Leseni ya Biashara Yako?

**Leseni ya Biashara**

Sajili duka lako kwa kupeleka maombi pamoja na ada inayohitajika kwa mamlaka husika. Stakabadhi zinazoweza kuhitaji ni pamoja na:

- maelezo yako binafsi, kama vile Kitambulisho (ID), paspoti, ithibati ya anwani, na vyeti vya kodi.
- maelezo kuhusu mipango yako ya shughuli za biashara, kama taarifa za malengo, Jinala Kampuni, mikataba ya kodi ya nyumba, au vyeti vya umiliki.

Hakikisha kufuatilia vitu vinayohitajika ili kuifanya leseni yako ya biashara kutumika. Vitu hivyo vinavyohitajika vinaweza kuwa pamoja na:

- kujaza fomu ya makato ya kodi kila mwaka.
- ulipaji wa kodi.

**Leseni ya Kuendesha Biashara**

Aina ya biashara yako, inaweza kuhitaji leseni ya kuiendesha ili kuhakikisha kuwa duka lako linafuata viwango vyoyte, masharti na kanuni za maadili na usalama. Stakabadhi zinazohitajika zinaweza kuwa:

- maelezo yako binafsi, kama vile Kitambulisho (ID), paspoti, cheti cha kodi, na cheti cha makazi.
- maelezo kuhusu biashara yako, kama vile cheti cha usajili, risiti za kodi, mikataba ya kodi ya nyumba, na ithibati ya anwani za biashara.

# Ulipaji Kodi

**Biashara zinahitajika kulipa kodi na kujaza fomu za makato ya kodi.** Hii inaweza kujumuisha kulipa kodi ya mapato kutokana na mapato ya biashara yako na kukusanya kodi ya mauzo kutoka kwa wateja wako.

Kujaza fomu ya makato ya kodi inaweza kufaidi biashara yako, na kulipa kodi ya mauzo inakufanya kuwa na ridhaa kwa sheria za serikali.



**FAIDA ZA KUJAZA FOMU YA MAKATO YA KODI:**

- ➔ Inatoa Kitambulisho (ID) cha kodi cha biashara yako
- ➔ Inatoa ithibati ya mapato na anwani
- ➔ Inatoa ufupisho wa rekodi za fedha bila kuwa na karatasi nyingi.
- ➔ Inakufanya wewe kustahili kodi ya akiba
- ➔ Inakuruhusu wewe kumaliziana deni kwa kulipa tofauti iliyopo au kuhamishia hasara mbele.
- ➔ Inatoa stakabadhi za kuidhinisha mkopo
- ➔ Inakusaidia kustahili kufanyiwa mchakato wa kadi ya mkopo
- ➔ Inakusaidia kuepuka adhabu za malipo

# Ruzuku za Kifedha Zinazopatikana kwa Wanawake Wanaomiliki Biashara



**Kuna mifano mingi ya ruzuku za kifedha zinazopatikana kwa wanawake wanaomiliki biashara, kama vile:**

- kupunguza viwango vya riba kwenye mikopo.
- punguzo la kodi kwenye mali.

# SEHEMU YA 4:
# KUENDESHA TATHMINI YA MAPUNGUFU KWENYE DUKA LAKO




**Malengo:**

1. Kuelewa ujuzi muhimu unaohitajika kuendesha duka.
2. Kujifunza jinsi wanawake na wanaume wanaweza kupata ujuzi unaohitajika kuendesha duka.

# Tathmini ya Mapungufu






**Wanawake na wanaume wanauwezo wa kufanya maamuzi ya biashara zao. Ujuzi wa kufanya maamuzi mazuri sio tabia ya kibayolojia. Yanaweza kupatikana kwa maarifa na mazoezi.**

Ikiwa unataka kubadilisha wajibu wako kwa biashara yako, nini kinahitajika kufanyika?

Mapungufu yako ni yapi kwenye ujuzi wako?

# Unataka Kupata Ujuzi Gani Kwenye Haya Mafunzo?




Sasa tuanze!

USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

STRATEGIC
IMPACT
ADVISORS



www.siaedge.com
Laini ya Pili
Laini ya Tatu

